


Mzunguko wa kabegi na kunde



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Masinde, AA

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

Kari-Kitale, S.L.P. 450, Kitale, 30200

Simu: (054) 201079

Fax: (054) 30378

Baruapepe: inmaktl@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 55 /2008

Shilingi Ishirini za Kenya

Kuza kabeji ukibadilishana na kunde kwa manufaa zaidi




Utangulizi

Kabeji hutoa mazao ya juu zaidi kwa gharama ya chini zikikuzwa kwa mtindo wa kubadilishana na kunde za kiafrika za kiasili (ALV) kama vile kunde na miroo/mitoo.

Kunde za kiafrika hutengeneza nitrojeni ambayo hufaidi mmea wa kabeji na kuongezea uzito wake kutoka kilo mbili hadi tatu kwa wastani, kwa aina zenye vichwa vidogo.

Majani ya kunde na miroo hutumiwa kama mboga na pia huandaa nitrojeni na kupunguza wadudu na kuwepo kwa maradhi.



Mmea wa kunde.

Mpangilio huu unawafaa wakulima katika sehemu zilizo na misimu miwili ya mvua, mchanga iliyotumika sana na kule ambako upandaji wa mmea mfululizo ni kawaida.

Jinsi ya kubadilishana kunde na kabeji

Hatua ya kwanza

Panda kunde za kiafrika au mitoo katika msimu mrefu wa mvua ifuatavyo:

Miroo: sentimita 45 kati ya misitari

Kunde: sentimita 45 kwa sentimita 20

- Tia gramu 180 (au mkebe mmoja wa gramu hamsini wa blue band) wa *Triple Super Phosphate (TSP)* kwa kila ploti ya mita 3 kwa mita 4.
- Chunguza kuchipuka kwa mimea ili kuhakikisha majani ya kutosha yatapatikana ya kufunika kwa mchanga.
- Hakikisha shamba lako halina kwekwe.

Hatua ya pili: Kuvuna majani

- Punde tu kabla ya mimea kuota maua, (miezi miwili na nusu baada ya kupanda), chuna majani na matawi yale mororo kwa kupikia au kuuza kama mboga.

Hatua ya tatu: Kuingiza mimea

- Kata matawi, majani na mizizi iliyosalia kwa vipande vidogo kisha uvitie mchangani kwa kuvilimia ndani.
- Wacha ardhi ipumue kwa muda wa mwezi mmoja hadi mmoja na nusu, huku ukitararisha mahali pa kupandia kabeji.

Hatua ya nne: Upandaji Kabeji

- Tayarisha shamba baada ya muda wa mwezi mmoja hadi mmoja na nusu.

- Tayarisha mashimo ya kupandia ukiacha nafasi ya sentimita 60 kwa sentimita 50 kisha utie kifuniko cha chupa kimoja hadi viwili vya mbolea ya *Phosphate*, hasa DAP kwa kila shimo.
- Panda mimea mchanga ya kabeji.
- Hakikisha hamna kwekwe shambani. Usitie mbolea ya juu isiyo asili kwa sababu si muhimu.

Hatua ya tano Kuvuna Kabeji

- Vuna kabeji baada ya siku 65 hadi 75 vichwa vikiwa vimejaa na imara kulingana na aina ya kabeji na sehemu zinapokuzwa.



Mmea ulionawiri wa kabeji

Manufaa

- Mboga za kiafrika (ALV) hutengeneza nitrojeni ambayo hutumiwa na kabeji na mkulima anfaidika kwa kutonunua mbolea ya nitrojeni kama vile CAN.
- Kuwepo wa mboga za kiafrika zingine (tani 3 kwa kila eka) juu ya kabeji.
- Kupunguzwa kwa wadudu na maradhi ambako kunaleta faida kwa kutopiga dawa.